WIZARA YA MAJI, USAFI NA UNYUNYIZIAJI
IDARA YA SERIKALI YA UNYUNYIZIAJI
HATI YA UTOAJI HUDUMA KWA WANANCHI

MAONO:

Kuwa na sekta kielelezo ya unyunyiziaji maji, ya kisasa na yenye kuleta mapato.

DHAMIRA/LENGO:

Kutoa mwongozo na kuwezesha ustawi na usimamizi wa unyunyiziaji maji hapa Kenya kupitia njia endelevu za utumiaji ardhi na rasilimali za maji ili kujitegemea kwa chakula na kufanikisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

MAADILI YA MSINGI:

Uwazi na Uwajibikaji; Utalamu na Udalifu; Ushirika Kazini; Shauku ya Matokeo; Kumpa Mteja Kipaumbele; Ushirikishwaji na Ujumuishwaji

S/No.	HUDUMA	KINACHOHITAJIKA	MALIPO	MUDA
1.	Kujibu simu rasmi	Kupiga simu	Bila malipo	Sekunde Kumi na Tano (15)
2.	Kujibu swali mteja anapofika ofisini	Fika ofisini na uulize swali	Bila malipo	Dakika moja
3.	Kujibu barua rasmi	Barua rasmi iliyoandikwa	Bila malipo	Siku Tano za kazi (5)
		Barua pepe na mitandao ya kijamii (X (awali ikijulikana kama Twitter) Facebook)	Bila malipo	Siku moja ya kazi (1)
4.	Kujibu malalamishi kutoka kwa umma	Toa malalamishi	Bila malipo	Siku moja ya kazi (1)
5.	Kusuluhisha malalamishi	Toa malalamishi kwa kuandika ama kwa kuongea	Bila malipo	Siku Kumi na Nne za kazi (14)
6.	Usajili wa watoaji huduma na wauzaji bidhaa	Jaza fomu za usajili Maelezo ya Kampuni yako Vyeti vya usajili wa kampuni, Cheti cha PIN, Cheti kilichoinidhinishwa cha ulipaji kodi.Taarifa ya Benki, Vyeti kutoka mashirika ya usajili wa vyama vya ubora wa huduma, Kitambulisho cha taifa ama hati ya usafiri	Bila malipo	Siku Kumi na Nne za kazi (14)
7.	Kushughulikia zabuni	Wasilisha stakabadhi za utoaji huduma ama uuzaji bidhaa	Bila malipo	Siku Tisaini (90)
8.	Kujulisha kuhusu waliofanikiwa na hawakufanikiwa katika zabuni hiyo	Tazama e- procurement portal ili ujulishwe	Bila malipo	Siku moja ya kazi (1)
9.	Kupokea malipo ya zabuni	L.P.O/stakabadhi ya kudai malipo, cheti cha ukamilishaji wa kazi na thibitisho kwamba bidhaa zimepokelewa na huduma imetolewa.	Bila malipo	Siku Sitini (60) baada ya kupokelewa kwa stakabadhi ya kudai malipo.
10.	Kuuza bidhaa zilizopitwa na wakati	Kupokelewa kwa stakabadhi za kuonyesha nia ya ununuzi.	Bila malipo	Siku Sitini (60) baada ya kuchapishwa kwa matangazo
11.	Ushirikishwaji wa umma katika kuunda sera	Kujifahamisha na maswala yaliyomo na kushiriki kikamilifu katika shughuli hiyo.	Bila malipo	Siku Moja (1)
12.	Kuajiri wafanyakazi	Andika barua rasmi kulingana na tangazo lililotolewa	Bila malipo	Siku Tisaini (90)
13.	Kushughulikia ombi la kupata habari	Andika barua rasmi ya kuomba upate habari au maelezo	Bila malipo	Siku Ishirini na Moja (21)
14.	Usajili wa watoaji huduma katika sekta ya unyunyiziaji maji	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi	Bila malipo	Mwezi Moja (1)
15.	Utoaji wa leseni kwa miradi ya unyunyiziaji maji na kujiandikisha upya	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi	Mradi mdogo- Ksh. 1,000 Mradi wa Wastani- Ksh. 3,000 Mradi mkubwa- Ksh. 5,000	Siku thelathini (30)
16.	Utadhmini kamilifu wa uwezekano wa kukomboa ardhi isiyotumika, kuteka maji na mirafi ya miundo mbinu ya uhifadhi wa maji	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi pamoja na ramani na data	Bila malipo	Miezi Sita (6)
17.	Simamia miradi ya miundo mbinu ya unyunyiziaji maji na ukombozi wa ardhi isiyotumika	Toa ombi ukieleza watakaonufaika na pia ushirikishwaji wa washika dau	Bila malipo	Inategemea na mradi unaoshughulikiwa
18.	Toa viwango vya ubora vya kubuni miundo mbinu ya miradi ya ukombozi wa ardhi isiyotumika na ya unyunyiziaji maji	Toa barua rasmi	Bila malipo	Mwezi Moja (1)
19.	Toa mafunzo kwa vitengo vya County Irrigation Development Units (CIDU) na mashirika ya Unyunyiziaji	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi la kutolewa mafunzo.	Bila malipo	Miezi Sita (6)
20.	Toa huduma ya kitaalamu ya kiufundi kuhusu miundo na viwango vya ubora katika unyunyiziaji na ukombozi wa ardhi isiyotumika	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi	Bila malipo	Inategemea na mradi unaoshughulikiwa
21.	Fanya tathmini na kuorodhesha viwango vya uharibifu wa ardhi	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi	Bila malipo	Miezi Sita (6)
22.	Shugulikia maombi ya miradi ya unyunyiziaji maji mashamba Kuendeleza miradi ya unyunyiziaji mdogo katika shule Uhifathi wa maji nyumbani mabawa madogo na unyunyiziaji mdogo katika shule	Tembelea tovuti ecitizen.go.ke na utoe ombi rasmi	Bila malipo	Mwaka Moja
23.	Toa data kuhusu unyunyiziaji maji na ukombozi wa ardhi isiyotumika	Toa ombi rasmi	Bila malipo	Siku Ishirini na Moja (21)

TUMEJITOLEA KUTOA HUDUMA BORA KWA UNYENYEKEVU

Huduma yoyote itakayotolewa ama bidhaa itakayouzwa ambayo haijalingana na viwango vya ubora vilivyoorodheshwa hapa vya utoaji huduma bora kwa unyenyekevu iripotiwe kwa :

Katibu
Wizara ya Maji,Usafi na Unyunyiziaji , Idara ya Serikali ya Unyunyiziaji
Maji House,
SLP 49720-00100, NAIROBI
DL: +254202733808
Email: ps@irrigationkenya.go.ke info@irrigationkenya.go.ke
public.complaint@irrigationkenya.go.ke

Mkurugenzi Mkuu Commission on Administrative
Justice, 2nd Floor, West End Towers, Waiyaki Way,
NAIROBI

Tel: +254(0)202270000/2303000
Email: complaint@ombudsman.go.ke

HUDUMA BORA NI HAKI YAKO